

6. Mikopo ya Maendeleo

Mikopo ya maendeleo imegawanyika katika sehemu mbalimbali kama vile kununua viwanja, ujenzi, magari, uwekezaji n.k. Kiwango cha juu cha mkopo huu ni mara tatu (3) ya Akiba na kutoza riba ya 0.84%. Muda wa kurejesha ni miezi 12-24. Kiwango cha juu cha mkopo kwasasa ni shilingi 10,000,000. Hutolewa mwanzoni wa mwezi kuanzia tarehe 1-5 ya kila mwezi. Masharti ya Mikopo ya ujenzi, magari na viwanja hutolewa utaratibu katika mkutano mkuu kutokana na fursa zilizopo katika bajeti ya mwaka ya SACCOS.

7. Kulipa riba akiba za wanachama

Chama hupokea na kutunza akiba za wanachama kupitia makato kwenye mshahara, au mwanachama anaweza kulipia bank kiasi chochote zaidi ya makato anayokatwa katika mshahara wake, aidha chama kinalipa 1% -5% ya akiba za mwanachama kama wanachama watakavyokubaliana kwenye mkutano mkuu.

8. Kutoa gawio kwa wanachama baada ya kupitishwa na mkutano mkuu Chama kitatoa gawio kwa wanachama baada ya kukubaliana kwenye mkutano mkuu.

9. Kutoa elimu ya ujasiriamali na uwekezaji kwa wanachama wake Chama kina utaratibu wa kutoa elimu ya ujasiriamali na uwekezaji kwa wanachama wake mara tatu kwa mwaka.

MWANACHAMA

Mwanachama wa DART WORKERS SACCOS ni mtu anayechangia akiba kila mwezi katika chama.

Je ni mtu yeyote anaweza kujiunga na DART SACCOS? Hapana ila ni mtumishi wa DART, mtu yoyote aliyeajiriwa sekta ya utumishi wa umma, mtu yoyote anayetokana na familia ya mtumishi wa DART i.e wenza na watoto.

JINSI YA KUJIUNGA NA DART SACCOS

Kujaza fomu ya kujiunga inayopatikana ofisi za DART WORKERS SACCOS LTD au kwenye tovuti ya chama.

1. Kulipa ada ya kiingilio 200,000 na

HUDUMA ZA KIFEDHA

Mwanachama anaruhusiwa kuweka Akiba (savings) au kulipa deni la DART WORKERS SACCOS LTD kupitia benki. Malipo yoyote yanayofanyika kwa mwanachama ni kwa njia ya kielektroniki kwenda kwenye akaunti yake.

UKOMO WA UANACHAMA

Kutokuweka akiba ndani ya miezi sita
Kuacha/kufukuzwa kazi serikalini

KANUNI YA KUTAFUTA RIBA

RIBA (Mkopo (Muda wakurejesha mkopo)

$$I = P(1+r) \times t / 200$$

MAADILI YA DART SACCOS

- Kufanya kazi kwa ubunifu, bidii na maarifa
- Uadilifu na uaminifu
- Kuendeleza mifumo Chanya yenye tija kwa chama
- Kutoa huduma bora yenye manufaa kwa wanachama
- Umoja na ushirikiano
- Uwazi na uwajibikaji
- Kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii
- Kupiga vita dhidi ya rushwa
- Kuheshimu usawa wa kijinsia katika uongozi wa SACCOS

WASILIANA NASI:

Ubungo Maji, Barabara ya Morogoro
S. L. P 80842, 16103 Dar es Salaam
Barua Pepe: info@dartsaccos.or.tz
Tovuti: www.dartsaccos.or.tz

f @dartsaccos



**DART WORKERS SAVINGS AND CREDIT
COOPERATIVE SOCIETY LIMITED.**
(DART SACCOS LTD)

DART WORKERS SAVINGS AND CREDIT COOPERATIVE SOCIETY LIMITED

ni chama kilichozanzishwa kwa madhumuni ya kustawisha na kuboresha hali za Maisha ya wanachama wake.

HISTORIA

Ushirika huu ulianzishwa mwaka 2022 ikiwa na wanachama 88 na kusajiliwa rasmi tarehe 30 Mei, 2023.

FUNGAMANISHO

Chama kinaundwa na

- Watumishi wa DART na mtumishi yoyote wa umma
- Familia ya mtumishi wa DART ambao ni wenza na watoto.



DIRA

Kuwa taasisi ya mfano Tanzania, inayotoa masuluhisho bora ya kifedha kwa wanachama wake.



DHAMIRA

Kuwezesha wanachama wetu kufikia malengo yao ya kifedha kwa kuwapatia bidhaa na huduma za akiba na mikopo ya bei nafuu, pamoja na elimu na mafunzo ya kifedha, ili waweze kujenga mustakabali mzuri kwao, familia zao, na jamii yao.

KWANINI UJIUNGE DART WORKERS SACCOS LTD?

DART WORKERS SACCOS inawahudumia watumishi wote wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), muajiriwa yoyote kutoka sekta ya utumishi wa umma, mtu yoyote kutoka familia ya mtumishi wa DART ambao ni wenza na watoto.

DART WORKERS SACCOS ni chama imara kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika, Sheria Namba 6 ya mwaka 2013, chenye malengo mapana ya kutoa huduma bora ya kifedha yenye lengo la kuwainua wanachama wake kiuchumi na kijamii kwa mujibu wa Sheria na kanuni za vyama vya ushirika.

DART WORKERS SACCOS hutoa huduma bora kwa wakati kama:

1. Kuuza hisa kwa wanachama
2. Kupokea na kutunza akiba na amana za wanachama
3. Kutoa mikopo ya dharura
4. Kutoa mikopo ya elimu (kulipia ada kwa wanachama, mtoto au tegemezi yeyote anayemuhusu mwanachama).
5. Mikopo ya biashara
6. Mikopo ya Maendeleo
7. Kulipa riba akiba za wanachama
8. Kutoa gawio kwa wanachama baada ya kupitishwa na mkutano mkuu
9. Kutoa elimu ya ujasiriamali na uwekezaji kwa wanachama wake.

BIDHAA NA HUDUMA ZINAZOTOLEWA:

1. Kuuza hisa kwa wanachama

a) Mwanachama atatakiwa kununua hisa kumi zenye thamani ya Shilingi 500,000/= ili kuruhusiwa kuwa mwanachama. Katika hatua za awali mwanachama ataruhusiwa kulipia angalau 50% ya hisa na hisa zilizobaki atapaswa kuzilipia ndani ya kipindi cha mwaka mmoja.

2. Kupokea na kutunza akiba na amana za wanachama

Chama hupokea na kutunza akiba za mwanachama zisizopungua Shilingi 50,000/= kila mwezi. Mwanachama ataruhusiwa kuingiza kiasi chochote kama akiba au amana kwenye akaunti ya mwanachama. Akiba za mwanachama zitatumika kama dhamana ya mkopo.

3. Kutoa mikopo ya dharura

Mkopo huu umegawanyika katika mafungu mbalimbali lengo ni kuhakikisha kila dharura ya mtu inatatuliwa kulingana na mahitaji ya mkopaji. Ili kuweza kutofautisha mikopo itakuwa inatambulishwa kwa majina tofauti ili kuleta uelewa na uhamasishaji kwa wanachama.

a) Mkopo wa dharura

Kiwango cha mkopo huu ni shilingi 1,000,000 na inatozwa riba asilimia 2% kwa mwezi. Muda wa juu wa marejesho ni miezi sita. Mkopo huu unatolewa ndani ya masaa 24 baada ya kukamilisha taratibu za maombi.

b) Mkopo hakuna Makasiriko

Kiwango cha chini cha mkopo huu ni Tsh 500,000/= na cha juu ni shilingi 800,000 na mwanachama atatozwa riba ya 5% kwa mwezi. Mkopo huu hurejeshwa ndani ya mwezi mmoja na hutolewa ndani ya dakika 20 baada ya kukamilika taratibu zote za maombi. Mwanachama atakapochelewesha kurejesha mkopo atapewa adhabu ya 1% kwa mwezi kama adhabu.

c) Mkopo wa Shangilia Wikiendi

Kiwango cha chini cha mkopo huu ni Tsh 100,000/= na cha juu ni shilingi 300,000 na mwanachama atatozwa riba ya 5% kwa mwezi. Mkopo huu hurejeshwa ndani ya mwezi mmoja na hutolewa siku ya ijumaa tu na baada ya kuomba ndani ya dakika 20 utapokea mkopo wako. Mwanachama atakapochelewesha kurejesha mkopo atatozwa riba ya 1% kila mwezi kama adhabu.

d) Mkopo wa Sikukuu

Kiwango cha mkopo huu ni shilingi 500,000/= na utatozwa riba ya 3%. Muda wa juu wa kurejesha mkopo huu ni miezi mitatu. Hutolewa kwa sikukuu za Eid zote, Krismasi na Pasaka.

4. Kutoa mikopo ya Elimu (kulipia ada kwa wanachama, mtoto au tegemezi yeyote anayemuhusu mwanachama).

Kiwango cha juu cha mkopo huu ni mara tatu ya hisa za mwanachama alizonazo na atatozwa riba ya 0.85. Kiwango cha juu cha mkopo kwasasa ni shilingi 10,000,000 muda wa kurejesha mkopo ni miezi 24. Mwanachama atapaswa kuthibitisha ni mkopo wa elimu na (3) ya Akiba na mwanachama hutozwa riba ya 0.84 %. Muda wa kurejesha ni miezi 12-24. Isipokuwa mwanachama atapata "grace period" ya siku thelathini Kiwango cha juu cha mkopo kwasasa ni shilingi 15,000,000. Hutolewa mwanzoni wa mwezi kuanzia tarehe 1-5 ya kila mwezi.